

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA  
YA UCHAGUZI, MHE. JAJI (MST) WA MAHAKAMA YA RUFAA  
DAMIAN LUBUVA KATIKA MKUTANO WA TUME NA VIONGOZI  
WA VYAMA VYA SIASA KATIKA HOTELI YA NEW AFRICA  
TAREHE 11/ MEI/2015**

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

**Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya  
Uchaguzi,**

**Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**

**Mkurugenzi wa Uchaguzi,**

**Watendaji wa Tume,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kuwakaribisheni wote katika mkutano huu muhimu wa kupeana taarifa juu ya mchakato wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu. Tunatambua mnayo majukumu mengi na ya muhimu lakini mmetambua umuhimu wa mkutano huu na mmefika kuhudhuria kama ilivyotarajiwa. Tume inafarijika sana kukutana nanyi siku ya leo na inawashukuru sana kwa

moyo mliouonyesha wa kuhudhuria mkutano wetu. Asanteni na karibuni sana.

### **Ndugu Viongozi wa Vyama Vya Siasa**

Leo Tume inakutana nanyi kwa mara nyingine tena ili kuwapa taarifa kuhusu maandalizi ya Uchaguzi Mkuu. Kama mnavyofahamu Tume inaendelea na zoezi la Uboreshajii wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Zoezi hili lilianza tarehe 23/2/2015 na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda tarehe 24/2/2015 katika Mji wa Makambako. Zoezi hili linaendela vizuri ambapo Tume imekwisha kamilisha Uandikishaji katika Mkoa wa Njombe, na hivi sasa zoezi la Uboreshaji linafanyika katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara na Iringa. Baada ya kupokea vifaa zaidi; Tume inatarajia kuendelea na zoezi la Uboreshaji katika mikoa ya Dodoma, Rukwa, Katavi na Mbeya kuanzia tarehe 15/5/ 2015.

Vile vile Tume itaendelea na zoezi hilo katika Mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida na Kagera kuanzia tarehe 19/05/2015.

### **Ndugu Viongozi wa Vyama Vya Siasa**

Mtakubaliana nami kuwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu umekaribia sasa, na moja ya majukumu ya Tume kwa mujibu wa Katiba ya nchi ni kugawa Majimbo ya Uchaguzi. Kwa maana hiyo, Tume inatarajia

kufanya zoezi la kuchunguza Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi na kuyagawa Majimbo hayo kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge.

Katika zoezi hilo la Ugawaji wa Majimbo ya Uchaguzi, Tume itazingatia vigezo mbalimbali vikiwemo Idadi ya Watu, Upatikanaji wa Mawasiliano, hali ya Kijiografia na vigezo vingine kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge ya Mwaka 2010.

### **Ndugu Viongozi wa vyama vya Siasa,**

Mtakumbuka kwamba kwa mujibu wa Katiba ya nchi, zoezi hili la ugawaji wa Majimbo hufanyika mara kwa mara au angalau mara moja baada ya miaka kumi. Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi zoezi hili lilifanyika kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na sasa tukiwa tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu mwingine ni wazi kwamba idadi ya Watu katika Majimbo imeongezeka na hivyo kuona kwamba iko haja ya kugawa Majimbo kwa mujibu wa Sheria.

### **Ndugu Viongozi wa Vyama Vya Siasa**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya zoezi hilo sio tu kwa kuzingatia idadi ya watu lakini pia itazingatia upatikanaji wa Mawasiliano inayojumuisha miundombinu yaani barabara, simu na vyombo vya habari kwa ajili ya kupata mwakilishi atakaye harakisha maendeleo katika eneo husika.

Pia, kuangalia hali ya kiuchumi kwa kuweka uwiano kati ya eneo moja na jingine katika kuharakisha maendeleo ikiwa ni pamoja na hali ya Kijiografia kwa lengo la kuweza kuleta uwiano kati ya eneo moja na jingine.

### **Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa**

Tume itazingatia pia ukubwa wa eneo husika katika zoezi hili la ugawaji wa Majimbo. Kama tunavyofahamu kuwa kuna maeneo/ Majimbo mengine ambayo ni makubwa ikilinganishwa na Majimbo mengine na hii inatokana na ongezeko la idadi ya watu katika maeneo hayo na hivyo kufanya hitaji hili kuwa kigezo kimoja wapo.

### **Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa**

Kwa kumalizia, Tume inapenda kuwahakikishia kwamba zoezi hili la ugawaji wa Majimbo litakamilika kwa wakati na Wananchi watajulishwa ili Vyama vya Siasa viweze kuteua Wagombea katika Majimbo hayo. Tume itatilia maanani michango yenu ya maoni na mawazo ya namna nzuri ya kutekeleza jukumu hilo.

**Kwa niaba ya Tume** ninapenda tena kuwashukuru wote kwa kuhudhuria mkutano huu licha ya majukumu makubwa mlionayo. Baada ya kusema hayo ninatamka sasa kuwa Mkutano wetu umefunguliwa.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**